

KUTABARUKU: MBUNDA MSOKILE 1950-1995*

M.M. Mulokozi
Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Bwana Philbert Kwirinus R. Mbunda, ambaye katika ulimwengu wa uandishi alijulikana zaidi kwa jina la Mbunda Msokile, alifariki hospitalini Muhimbili tarehe 31/1/1995. Alizikwa kijiji kwa Liule-Unago, Mbinga, tarehe 4/2/1995.

Jina la Mbunda Msokile lilikuwa mashuhuri sana nchini Kenya na Tanzania, hasa mionganoni mwa vijana. Alijulikana pia katika ulimwengu wa taaluma ya Kiswahili. Umashuhuri huu aliupata kutokana na juhudi zake za uandishi: ametuachia jumla ya vitabu 5 vya hadithi za kubuni, vitabu 6 vya taaluma ya lugha na fasihi, vitabu 8 vya miongozi ya fasihi, miswada 6 iliyokamilika na labda hadithi na makala fupi zaidi ya 100 zilizochapishwa katika vitabu na magazeti mbalimbali. Ni wasomi wachache sana nchini Tanzania hivi leo waliota machapisho mengi kiasi hicho. Hivyo kifo chake ni pigo kubwa kwa fasihi na mitaala ya Kiswahili, na kwa utamaduni wa Tanzania kwa jumla.

Mbunda alizaliwa katika kijiji cha Mkumbi-Liule, Mbinga, Mkoa wa Ruvuma, tarehe 20/2/1950. Alikuwa ni mtoto wa tatu mionganoni mwa watoto 11 wa Mzee Kwirinus Mbunda (ambaye sasa ni marehemu) na mkewe, Bi. Rosalina Mwingira. Mbunda alikulia katika mazingira yenye ushirikiano na uchangamfu, na alidumu na tabia hiyo ya uchangamfu na ucheshi hadi kifo chake. Mbunda alisomea katika Shule ya Msingi ya Wukiro, Mbinga (1959-1962), Shule ya Kati ya Litembo (1963-1966), Shule ya Sekondari ya Kigonsera (1967-1970) na Shule ya Sekondari ya Ihungo (1971-1972). Alijunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwezi Julai mwaka 1973, na kufuzu digrii ya B.A. pamoja na Ualimu mwaka 1976. Alipangiwa kufundisha kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Masasi.

Mbunda alioa mara mbili. Ndoa yake ya kwanza, kwenye miaka ya 1980, haikudumu. Mwaka 1992, Mbunda alimwoa Bi Joyce Antony ambaye pia ni mwalimu. Hadi alipofariki, walikuwa wamekwisha pata watoto wawili.

Mara tu baada ya kuanza kufundisha Masasi, Mbunda aliteuliwa kuwa mkuu wa idara ya Kiswahili na kitengo cha malezi na utamaduni shulenii hapo. Wakati huo ndipo kipaji chake cha utunzi kilipodhihirika: Alianza kuchapisha hadithi fupi na makala nyingi katika magazeti ya Kiswahili, hususan **Nchi Yetu, Mzalendo na Kiongozi**. Kadhalika, alitunga riwaya kadha.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilivutiwa na juhudi za Mbunda katika utunzi na taaluma, na mwezi Aprili mwaka 1979 ikamwajiri kama Mkufunzi Msaidizi chini ya mpango wa kuazimwa kutoka Wizara ya Elimu. Mwezi Aprili

* Tunawashukuru Bw. Walter M. Mbunda, mdogo wa Marehemu Mbunda Msokile, na Mkurugenzi wa Matibaa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DUP), kwa kutupatia baadhi ya taarifa zilizomo katika tabaruku hii.

1992, Mbunda alihamishiwa katika Matibaa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DUP) na kuwa Mhariri. Kutokana na juhudhi yake, alipandishwa cheo hadi kuwa Meneja wa Masoko wa Matibaa mwaka 1992. Huo ndio wadhifa aliokuwa nao wakati alipofariki.

Licha ya majukumu mazito ya kiuchapishaji aliyo kuwa nayo, Mbunda aliendelea na shughuli yake ya utumzi na uandishi wa makala. Alifululiza kuandika vitabu vya taaluma, insha, makala ya magazetini, riwaya na visa.

Si nia yetu kufanya tathmini ya machapisho yake ya kisanaa na kitaaluma katika kumbukizi hii. Tuwezalo kulisema hapa ni kwamba kama ipo "fasihi pendwa" yenye uzito, basi hadithi za Mbunda zastahiki kupewa heshima hiyo.

Dhamira kuu za hadithi za Mbunda huhusu migogoro ya kinyumba, hususan matatizo ya ndoa na uasherati (riwaya ya **Dhihaka ya Mume**), matatizo ya mapenzi mionganoni mwa vijana wanaoanza kubalehe (hadithi fupi imbalimbali), matatizo ya kukua kwa miji na vijana wasio na kazi (**Usiku Utakapokwisha**), rushwa na ufisadi wa wakubwa, kusalitiwa kwa Uhuru, na haja ya kupigania "Ukombozi wa Pili" (**Thamani ya Ukubwa na Pambazuko**). Maandishi ya Mbunda ni rahisi kueleweka, yana mvuto kwa wasomaji wa kawaida, yanagusa nafsi kihisia, yanasisimua, na yanachokonoa masuala na kuelimisha.

Mbunda alikuwa ni mwalimu na mwenezaji wa taaluma ya juu kwa Umma. Katika maandishi yake ya kitaaluma, kama katika hadithi zake, alijaribu kuwasiliana na wasomi wanaoinukia, wanafunzi na walimu wa shule za sekondari, wanafunzi wa vyuo vikuu, na wananchi kwa jumla. Aliliandikia kundi la watu ambalo kwa kawaida halishughulikiwi vilivyo na wataalamu wetu.

Uhamisho wa Mbunda kutoka TUKI kwenda DUP ulikuwa na athari moja nzuri ambayo haikukusudiwa: ulimtoa katika kifungo cha masharti ya uanataluma wa kidhahania na kumruhusu kutumia vipaji na utaalamu wake ku wahudumia wale waliouhitaji zaidi. Alijikuta akiba kiungo kati ya akademia na Umma. Ujuzi wake wa ulimu aliendelea kuutumia kuelimisha na kueneza maarifa mapya kwa umma kwa kipindi chote kifupi cha maisha yake.

Katika kiwango cha kitaifa, Msokile aliwakilisha hamu ya Tanzania ya kujitambulisha na kujieleza kitaifa na kitamaduni. Daima aliandika katika lugha ya Kiswahili, na hivyo kuchangia katika ukuzaji wa Kiswahili kama lugha ya fasihi na taaluma za juu. Labda alielewa kuwa utambulishi na heshima ya taifa lolote lile imefungamana na lugha. Na hii ni kweli ambayo kwa bahati mbaya wasomi wengi wa Kiafrika hawajaibaini.

Hatuwezi kutoa hapa orodha ya machapisho na maandishi yote ya Mbunda Msokile kwa kuwa maandishi yake bado yanakusanya. Hivyo orodha ifuatayo ni sehemu tu ya hazina kubwa aliyo tuachia:

Hadithi za Kubuni

1. **Pambazuko** (EAPH 1975)
2. **Dhihaka ya Mume** (Meza Publications 1979)
3. **Thamani ya Ukubwa** (Meza Publications 1979)
4. **Nitakuja kwa Siri** (Mkusanyo wa visa) (DUP 1981)
5. **Usiku Utakapokwisha** (DUP 1990)

Hatukufanikiwa kupata orodha kamili ya visa (hadithi fupi) alivyovitunga: tunakadiria kuwa havipungui 50.

Maandishi ya Kinadharia

1. **Fasihi Simulizi ya Mtanzania (na wenzake, TUKI)**
2. **Uhakiki wa Vitabu vya Fasihi (na wenzake)**
3. **Misingi ya Hadithi Fupi (DUP, 1992)**
4. **Historia na Matumizi ya Kiswahili (EPD, 1992)**
5. **Kunga za Fasihi na Lugha (EPD 1992)**
6. **Misingi ya Uhakiki wa Fasihi (EAEP, Nairobi, 1993)**

Bado tunajaribu kukusanya na kuorodhesha kazi zake za kitaaluma.

Miongozo ya Fasihi

1. **Jiandae na Fasihi: Kidato cha Sita (EPD-hakijatoka)**
2. **Uhakiki na Uchambuzi wa Lina Ubani (DUP 1991)**
3. **Uhakiki na Uchambuzi wa Karibu Ndani (DUP 1991)**
4. **Uhakiki na Uchambuzi wa Harusi (DUP 1991)**
5. **Uhakiki na Uchambuzi wa Fungate Uhuru (DUP 1991)**
6. **Uhakiki na Uchambuzi wa Riwaya, Kidato cha 4 (DUP 1993)**
7. **Uhakiki na Uchambuzi wa Ushairi, Kidato cha 4 (DUP 1993)**
8. **Uhakiki na Uchambuzi wa Tamthiliya, Kidato cha 4 (DUP 1993)**

Miswada

1. **Miongozo ya Lugha na Fasihi: Mashairi ya Cheka Cheka**
2. **Fasihi Simulizi: Mbinu na Misingi Yake**
3. **Ngoma ya Wanyama (hadithi ya watoto)**
4. **Miongozo ya Lugha na Fasihi: Mashetani na Ushuhuda wa Mifupa.**
5. **Mashaka ya Sungura (hadithi ya watoto)**
6. **Jogoo Mfalme wa Ndoto (hadithi ya watoto)**

Apumzike kwa amani

**Mashairi
Tukutane Katikati**

Panda mlima nishuke
Panda mlima nishuke
Tukutane katikati

Jogoo limesha wika
Na tembe linatetea
Dume nalo linatamba
Na mtamba acharuka

Umeshashuka bondeni
Na maji umeyateka
Nami niko kilimani
Mkuki nimeushika
Na kibuyu cha maziwa

Panda mlima nishuke
Shuka mlima nipande
Tukutane katikati

Halafu tufuatane
Halafu tushikamane
Hadi kule kileleni
Wewe na mtungi wako
Mimi na kibuyu changu

Ndipo maji ya uzima
Uyatose niyaoge
Nami maziwa ya ne'ma
Niyarushe uyameze:
Tunywe pamoja mpenzi
Hayano ndiyo maisha!

**M.M. Mulokozi
1994**

Nduli

Uchuro: Waangamiza dunia!
Kihoro: Wapata wenyewe kuzaa!
Inda: Wachukia wenyewe raha!
Machelia: Wabeba watu wazima
Wingu: Waziba mwanga wa juu!
Ilani: Watangaza kufa fofo!

**M.M. Mulokozi
1994**

Wapanda Mlima

Tulianzia bondeni
Kunako jua jekundu
Tuliupanda mlima
Kwa hatua za haraka
Kwa pumzi za hakika
Nguvu zikiongezeka
Uwezo ukizidika
Vifua vikipanuka
Kadiri tunavyopanda

Tumefika kileleni
Kwenye jua la utosi
Tumevuka makorongo
Tumekwea majabali
Sasa twasimama juu
Ya chini twaangalia

Nyuma twaona hatua
Zinapotea bondeni
Mbele twaona hatua
Zinapotea bondeni

Juu ni moto wa jua
Na bahari ya samawi
Ni shani kuangalia

Sasa twavaa miwani
Na kubadili kofia
Twaanza kuteremka
Huku twavuta haṭua
Tunapumua kwa shida
Nguvu zinatufifia
Vifua vinapungua
Kadiri tunavyoshuka
Kuelekea bondeni
Kwenye ukingo wa kiza

**M.M. Mulokozi
1995**